Stanbic Bank

BENKI YA STANBIC MAELEZO NA MASHARTI YA MTANDAO WA KIELEKTRONI

1. Mkataba na Ridhaa

Mkataba huu unaanza kutumika baina ya mwombaji ("**wewe" au "wako**") na Benki ya Stanbic Tanzania Limited (yaani "Benki", au "**Sisi**") wakati wa usajili wa kutumia huduma za kielektroni za Benki au wakati unapotumia huduma za kieletroniki za Benki kwa chochote kinachotangulia. Kwa mujibu wa mkataba huu "huduma za kielektroni za benki" zinajumlisha matumizi ya benki kwa Intaneti, huduma za benki kwa simu (programu ya simu ya kiganjani na Data ya Huduma ya Ziada Isiyo Rasmi (USSD*150*20#) , na huduma au bidhaa za malipo ya awali zilizonunuliwa au kutumiwa kupitia benki mtandaoni au benki kwa simu.

2. Masharti Unganishi

Pamoja na mkataba huu, maelezo na masharti ya kadi yako na akaunti au maelezo na masharti ya uwezeshaji (masharti mengine) yatatumika kwa miamala yote unayofanya au kutuelekeza kufanya kupitia akaunti za benki zilizounganishwa na kadi yako. Iwapo masharti ya kadi ya benki au masharti mengine yanahitaji marekebisho au nyongeza kufanyika kwa maandishi na/au kutiwa saini, ridhaa yako ya mkataba huu itachukuliwa kutosheleza masharti hayo.

3. Kuelezea Kifaa na Utaratibu

Kifaa unachochagua kutumia huduma za kielektroni za benki kinaweza kuwa kompyuta, simu ya kiganjani, kadi ya simu, simu ya mezani, televisheni au teknologia kama hizo (kifaa), na utaratibu ambao unatumia kupata huduma za benki za kielektroni unaweza kujumlisha Intaneti, Itifaki ya Maombi ya Upepo (WAP), Huduma ya Jumbe Fupi (SMS), Huduma ya Data ya Nyongeza (USSD), sauti kupitia mfumo wa utambuzi wa sauti unaojiendesha au teknolojia nyingine za aina hiyo. (utaratibu). Kwa pamoja tutarejea kifaa na utaratibu kama "mfumo wa mawasiliano". Iwapo mfumo mwingine wa mawasiliano mahsusi unahitaji vipengele vya mkataba tofauti na mifumo mwingine ya mawasiliano, hili litaelezwa kwa uwazi katika mkataba huu.

4. Matini unganishi

Kwa Kurahisisha matumizi, tumeweka viunganishi vinavyojiendesha (hyperlinks) katika Mkataba huu ambavyo vinaweza pia kupatikana katika mfumo wako wa mawasiliano. Viunganishi hivi vina rangi ya maandishi ya bluu na kivinjari chako kibadilike kuwa mkono au kiashiria kingine kinaposhikiliwa kwenye maandishi hayo. Unatakiwa kuangalia sehemu zinazohusika za taarifa unganishi ambayo itachukuliwa kuwa sehemu ya mkataba huu. Iwapo mfumo wako wa mawasiliano hauwezi kutumia viunganishi hivi, inabidi utumie tovuti ya www.stanbicbank.co.tz kupata taarifa unganishi au Kituo cha Huduma kwa Wateja kwa kutumia Namba ya Bure: **0800751111** na Barua pepe: tanzaniaccc@stabic.com.

5. Marekebisho

Marekebisho katika sheria, teknologia na maboresho ya huduma yatahitajika kwamba maelezo na masharti yabadilishwe mara kwa mara.

Kwa hiyo tuna haki ya kubadilisha maelezo na masharti baada ya kukupatia taarifa. Ikiwa tutabadilisha maelezo na masharti hayo yatachapishwa katika mfumo wa kielektroni wa benki au vinginevyo na kuchukua nafasi na ya matoleo yote ya awali. Muda wote ni wajibu wako kuhakikisha unaelewa na kuheshimu maelezo na masharti mapya.

6. Masharti na Usajili

Kabla ya kutumia benki ya kielektroni unatakiwa kufuata hatua fulani.

6.1 Intaneti, Programu ya simu ya Kiganjani na Huduma ya Benki USSD

Kwanza sharti ujisajili katika tawi lako la karibu kwa kujaza fomu ya usajili kwa mkono au mtandao kwa kutumia usajili wa akaunti Binafsi inayopatikana kupitia kiungio https://funguaaccountstanbicbank.co.tz au unaweza kujisajili kupitia msimbo mfupi wa Huduma ya Benki ya Mtandaoni. Utapokea nywila ya muda mfupi ambayo sharti uibadilishe mara unaposajili nywila yako. Kusajili kwa kutumia bio metriki (utambuzi wa vidole/uso), unaweza kutumia utaratibu huu kupitia Programu ya Simu.

6.2 Programu ya Simu/Mfumo Benki wa WAP

Unaweza kutumia jina la mtumiaji na nywila za benki mtandaoni kuingia kwenye Programu ya Stanbic au huduma ya benki kupitia WAP.

Uthibitishaji

Huwezi kuanzisha nywila kwa kutumia maelezo ya mtu mwingine. Kabla hatujakuruhusu kutumia mfumo wa benki wa kielektroni tunaweza kuhitaji taarifa kutoka kwako ili kufanya ukaguzi juu yako kabla ya kuchakata maelekezo.

7. Huduma

7.1 Ni wajibu wako mwenyewe kujua taratibu za utumiaji wa huduma kadiri itakavyotolewa na Benki baada ya kujisajili katika huduma yenyewe. Benki haitawajibika kwa hasara yoyote kutokana na kukosea kwa kufanya au kutofanya.

7.2 Unaridhia na kuahidi kuwajibika na kutekeleza taratibu zote kadiri zitakavyotolewa na Benki kila inapobidi. Benki haitawajibika na au kulazimika kuchukua hatua zozote kuhusu maelekezo ambayo hayaendani vizuri na taratibu na Benki inaweza kukataa maelekezo hayo yanayopingana na taratibu.

7.3 Utoaji na kiwango cha huduma utategemea upatikanaji wa viunganishi vinavyotumika kupata huduma ya kielektroni ya Benki. Benki haitawajibika kwa kushindwa au kuchelewa kutoa au kutoa huduma kwa makosa kutokana na kuathirika kwa viunganishi.

7.4 Hatutawajibika kwa kosa lolote linalosababisha kupatikana kwa taarifa ambayo sio sahihi.

7.5 Benki itahakikisha kadiri inavyowezekana kwamba taarifa yoyote inayotolewa kwako kupitia huduma hii ni sahihi. Hatutawajibika kwa kosa lolote linalosababisha kupatikana kwa taarifa ambayo sio sahihi.

7.6 Unakubali hatari na matokeo yoyote ya kushindwa kutuma na au kutekeleza maelekezo yoyote yaliyotumwa kwa kutumia huduma hii kutokana na makosa katika utumiaji wa maelekezo yako.

7.7 Unaahidi kutunza kifaa chako vizuri. Usiache kabisa kifaa chako bila uangalizi au kuruhusu mtu yeyote kukitumia kwa namna yoyote ile na/au kwa huduma ya kielektroni ya Benki, iwe kwa ruhusa au bila ya ruhusa yako.

7.8 Lazima uiarifu Benki mara moja kuhusu wizi au kupotea kwa simu yako ya kiganjani/sim kadi, matumizi yoyote yasiyoruhusiwa ya huduma au kutokana na kukatishwa kwa huduma ya simu na mtoaji wa huduma hiyo, kupitia Kituo chetu cha Huduma kwa Wateja. Benki haitawajibika kwa hasara zozote kutokana na kupotea kwa sim kadi na/au simu ya kiganjani kwa vyovyote vile. Benki haitawajibika iwapo namba ya siri inatolewa kwa mtu mwingine, haionekani, au imepotea kwa namna au njia yoyote.

7.9 Benki inabaki na haki ya kuongeza huduma wakati wowote bila taarifa kwako. Ni wajibu wako kufuatilia maendeleo haya. Benki itafanya jitihada zote kukufahamisha mabadiliko au taarifa zozote.

7.10 Lazima uiarifu Benki mabadiliko yoyote kuhusu namba ya Akaunti yako, anuani na taarifa yoyote inayoweza kuathiri uwezo wako wa kutumia huduma hii. Benki haitawajibika kwa kutuma taarifa kwenye namba ya simu yako ya kiganjani ambayo iko katika kumbukumbu zetu wakati wowote ule.

7.11 Unaweza kujitoa katika Huduma kwa kuwasiliana na sisi kupitia chaneli zetu za Huduma kwa wateja kusitisha huduma hii.

8. Ada

Utawajibika kuilipa Benki kwa ada yoyote inayotozwa kwa utumiaji wa Huduma isipokuwa kama Benki kwa ridhaa yake yenyewe imeondoa ada hiyo. Kwa kukubali maelezo na masharti haya unaipa Benki mamlaka ya kutoa ada hizi kutoka akaunti yako kwa wakati ambapo miamala inafanyika. Tozo hizi zitakuwa ada kwa ajili ya Huduma hii kila inapohitajika kwa kutoa taarifa kama inavyohitajika na sheria. Benki ina haki ya kutengua mkataba iwapo utashindwa kulipa ada yoyote inayotozwa kwa utoaji wa Huduma. Benki ina haki ya kutoza ada kwa utoaji wa Huduma na muda.

9. **Tutatekeleza maelekezo yaliyotumwa na wewe**

Matumizi ya mfumo wa mawasiliano maana yake hatuonani uso kwa uso. Usipotupa taarifa kabla ya utekelezaji basi unaturuhusu tuendelee kutekeleza maelekezo yote yanayoonekana kutoka kwako (hata kama kuna mtu anajifanya kuwa wewe).

10. Utumiaji na utekelezaji maelekezo

Maelekezo yako ya matumizi yatafanyika kutokana na muda ule ule wa kutekeleza maelekezo. Maelekezo, pamoja na malipo ya bidhaa zilizolipwa kabla, hayawezi kusitishwa au kufutwa baada ya kutumwa kwetu. Hutatuwajibisha iwapo utatuma maelekezo yale yale kabla ya kuyahakiki au kuuliza huduma yetu ya wateja hivyo kuweza kusababisha kufanya miamala miwili.

11. Kuthibitisha upokeaji wa maelekezo yako

Maelekezo yatahesabiwa kupokewa na sisi pale tu tutakapothibitisha kuyapokea. Iwapo hatutathibitisha upokeaji wa maelekezo yako usitume tena maelekezo hayo kabla ya kuangalia mahesabu yako au kuuliza Kituo chetu cha Huduma kwa Wateja. Hii ni kwa sababu maelekezo ya kwanza yanaweza kusababisha miamala miwili ambayo hatutawajibika nayo.

12. Ulinzi wa Mzimbo wa matumizi na hitilafu

“ Mzimbo wa matumizi “ ina maana ya nywila yako na jina lako la matumizi. Sharti ukinge kompyuta yako au vifaa vingine vya kielektroni unapotumia huduma hizi. Tunakutegemea utuarifu matatizo yoyote ya matumizi ya mzimbo wako bila kuchelewa. Unaweza kufanya hivyo kwa kupigia Kituo chetu cha Huduma kwa Wateja au tawi lako. Tunaweza kukuomba uhakiki kitambulisho chako ili kuzuia mtu mwingine asijifanye wewe.

13. Mara unapotuomba tusitumie msimbo wako wa matumizi tuna haki ya:

a. Kukataa maelekezo yote yaliyopokelewa baada ya taarifa hiyo.
b. Sitisha uchakataji wa maelekezo yote ambayo hayajatekelezwa.

c. Kubadilisha (ikiwezekana) maelekezo yote yaliyotekelezwa kutoka tarehe na wakati unaohusika na kadiri tutakapojua utekelezaji ambao haukuruhusiwa ulipoanza; na
d. Kutotumia mzimbo wa matumizi bila ya taarifa yoyote ya ziada.

Hakutakuwa na sababu yoyote kwa mtu yeyote, pamoja na watumishi wetu au wa Kituo cha Huduma kwa Wateja, kujua au kuomba matumizi ya mzimbo wako. Sharti utufahamishe mara moja unapogundua kosa au hitilafu. Unaweza kutoa taarifa ya makosa yoyote kwa Kituo chetu cha Huduma kwa Wateja au tawi lolote.

14. Nywila ya wakati mmoja

Hii ni nywila ya kipekee yenye kuzingatia muda inayotumika kama nyongeza ya usalama katika benki ya kielektroni. Nywila hii sio mbadala wa nywila unayoitumia katika benki ya kielektroni lakini huweka nyongeza ya pili ya usalama. Nywila itatumwa mara moja tu kwa intaneti ya kibenki. Nywila ya wakati mmoja (OTP) inatumika kwa ajili ya:

a. Matumizi ya mara ya kwanza
b. Kuongeza wanufaika
c. Kurekebisha wanufaika; na
d. Ubadilishaji nywila yako
e. Kufanya malipo (Huduma za Nyongeza za Thamani)

15. Kumaliza muda

Lazima uhakikishe unajiondoa kutoka huduma ya benki ya kielektroni.

16. Ruhusa Yako

Unaturuhusu kuona kwamba shughuli zote unazotenda au maelekezo yaliyotumwa baada ya kuingiza msimbo wa matumizi vimeidhinishwa na wewe na kukusudiwa kuwa na nguvu ya kisheria na utekelezaji.

17. Taarifa ya kutosha

Unaturuhusu kutoa taarifa zinazotakiwa mujibu wa mkataba huu, kwa kufanya taarifa hiyo kupatikana kupitia mfumo wetu wa mawasiliano au kwa barua pepe, SMS. Taarifa hizo zilizotolewa na sisi kadiri zitakavyokuwa na masharti ya mkataba kuhusu benki ya kielektroni, zitakuwa sehemu ya mkataba huu.

18. Hakuna kadimisho, mapendekezo au ushauri

Isipokuwa inapoelezwa wazi, maelekezo yote katika mfumo wa mawasiliano ni chombezo tu la kufanya biashara na sisi. Sio kadimisho au ushauri kununua au kuuza au kuacha kwa namna yoyote uwekezaji au kuingia katika muamala wowote.

19. Aina ya taarifa katika mfumo wa mawasiliano

Taarifa katika mfumo wa mawasiliano inakusudiwa tu kukupatia taarifa ya jumla kuhusu Benki, bidhaa zake, huduma na malengo yake. Mara kwa mara tunaweza kutoa taarifa kuhusu:

a. Makusanyo yanayotegemewa, mapato, mapato kwa hisa, matumizi ya mtaji
b. Mipango yetu, malengo na matarajio kwa miradi na huduma za baadaye na
c. Utendaji wa baadaye kiuchumi. Haya yatakuwa makadirio, kwa hiyo matendo au matokeo halisi yanaweza kutofautiana.

Taarifa yote inatolewa ‘kama ilivyo’ na isichukuliwe kama ushauri wa kitaalamu au uwekezaji wa aina yoyote ile. Pata ushauri wa wataalam wako kabla ya kutegemea

taarifa yoyote katika mfumo wa mawasiliano.

20. Mahitaji ya Taarifa

Tunaweza kutumia huduma za mashirika mengine kutoa taarifa kuhusu mfumo wa mawasiliano. Hatuna udhibiti wa taarifa hizi na hatutoi uwakala au dhamana ya aina yoyote kuhusu usahihi, uhakiki au usawa wake. Unakubali kuwa taarifa hiyo inatolewa "kama ilivyo" na hatutawajibika moja kwa moja au kwa njia nyingine kwa hasara itakayotokea kutokana na wewe kuitegemea. Madondoo, habari za taarifa za masoko kama vile bei za hisa au data iliyoonyeshwa katika mfumo wa mawasiliano kwa kutumia taarifa mubashara zinacheleweshwa kwa japo dakika thelathini isipokuwa inapoelezwa vinginevyo. Siku zote chagua ukurasa wa " kumbukumbu" au mfumo wake au kiboresha *skrini* katika kirambaza cha intaneti au simu ya kiganjani kuhakikisha kwamba taarifa unayoiangalia ndiyo ya wakati uliopo.

21. Viunganishi kwenye mifumo ya mawasiliano ya watu wengine

Mfumo wa mawasiliano unaweza ukawa na viunganishi na mifumo mingine ya mawasiliano yenye taarifa na maudhui yanayotayarishwa na watu wengine. Wakati tunajitahidi kutoa viunganishi kwa mifumo ya mawasiliano inayoaminika tu, hatutawajibika kwa taarifa inayotolewa kwenye mifumo ya mawasiliano mingine. Kiunganishi kutoka mfumo wetu wa mawasiliano kwenda kwenye mifumo mingine ya mawasiliano haina maana tumechunguza au kuidhinisha wenye mifumo hiyo au biashara, taratibu zao za kiusalama na shughuli zao.

22. Miliki yetu ya ubunifu

Tunabaki na haki miliki na haki za miliki ya ubunifu katika taarifa, pamoja na nembo na michoro na kazi za vyombo vya habari zilizochapishwa kwenye au kupitia mfumo wa mawasiliano. Unaruhusiwa kuangalia na kupakua nakala moja kwa maunzi ngumu au diski, chapisho au kutoa nakala za machapisho hayo alimuradi tu:

a. Habari zinatumika kwa kutafakari au kutumia huduma ya benki ya kielektroni na sio kwa matumizi mengine ya kibiashara;
b. Kurudufu kokote kwa sehemu ya taarifa yetu sharti ijumlishe taarifa yote ya haki miliki; na
c. Nembo ni alama za biashara zinazoonyeshwa katika mfumo wetu wa mawasiliano, ni alama za biashara zilizosajiliwa au kutosajiliwa au za watu wengine.

23. Uwezo wa utendaji wa maunzi laini

Kushindwa kwako kutumia maunzi laini au maunzi magumu kunaweza kusababisha hatari ya kiusalama kubwa na kusababisha mfumo wa mawasiliano kutofanya kazi vizuri au kushindwa kabisa. Maunzi laini, yakiwepo tayari kwa kupakua kwenye au kupitia mfumo wa mawasiliano, unasimamiwa na masharti ya leseni yanayoweka uhusiano wa kisheria na mtoa leseni. Unatufidia kwa ajili ya ukiukaji wa masharti haya ya leseni. Hatutoi uwakala au dhamana kwamba maombi kupitia mfumo wa mawasiliano hayana virusi, trojani, mabomu, vifungo vya muda au data nyingine au msimbo ambao unaweza kuharibu au kuingilia utendaji wa hazina data ya kompyuta yako, mtandao au mfumo wa taarifa mwingine.

24. Utoaji wa taarifa na vionyo vya usalama

Taarifa iliyotumwa kupitia kiungo kisicholindwa kwenye mfumo wa mawasiliano ina hatari ya uwezekano wa matumizi haramu, upotoshaji au ufuatiliaji. Lazima ufuate vionyo vya usalama vinavyochapishwa kwenye tovuti mara kwa mara. Kwa vile hatuna uwezo wa kuzuia vitendo haramu vya watu waovu, unaridhia kwamba hatutawajibika kwa hasara, uharibifu au upotevu wowote ulioupata kutokana na, taarifa yoyote unayotuma kupitia mfumo wetu wa mawasiliano mara kwa mara.

25. Fidia

Unatufidia kwa hasara na gharama zote tunazoweza kulipa kwa niaba yako kutokana na:

a. Kutolipa;
b. Maelekezo au muamala wowote unaozidi kiasi ambacho kiko katika akaunti yako ya benki; au
c. Maelekezo ambayo hayakuidhinishwa yaliyotekelezwa bila ya uzembe wetu.

26. Katao la dai na ukomo wa deni

Kwa mujibu wa ibara hii “sisi” au “ yetu” inajumlisha Benki. Hatuwajibiki kwa hasara yoyote kuhusiana na matumizi ya mfumo wa mawasiliano au huduma za benki ya kieletroni isipokuwa pale hasara hiyo imetokana na uzembe uliothibitika au wizi wa watumishi wa Benki. Hii inajumlisha taarifa ambayo iko katika mfumo wako wa mawasiliano au kushindwa kwako kutumia mfumo wa mawasiliano au huduma ya kieletroni ya benki; pamoja na, bila ya ukomo, hasara zozote za moja kwa moja au la zilizosababisha au kusababishwa, iwe zinatokana na mkataba, sheria, kosa (ukiukaji) au vinginevyo na bila kujali iwapo tulielezwa waziwazi kuhusu uwezekano wa hasara au uharibifu huo. Bila kuathiri yaliyotajwa hapa juu, hatuwajibiki kwa:

a. Uharibifu wowote unaoupata kutokana na athari ya misimbo ya matumizi yako;
b. Kuingiliwa, kutofanya kazi, ucheleweshaji au uharibifu wowote wa mfumo wa mawasiliano au huduma ya benki ya kieletroni, mifumo ya watu wengine, hazina data au sehemu yoyote inayohusika kwa sababu yoyote;
c. Hasara au uharibifu wowote unaotokana na maelekezo yako, uamuzi wa kuwekeza au fedha kutoka watu wengine kutokana na taarifa inayopatikana kwenye mfumo wa mawasiliano;
d. Hasara au uharibifu wowote kuhusiana na data yako au nyingine ambao moja kwa moja au sio moja kwa moja uliosababishwa na kuharibika kwa mfumo wetu wa Benki, mifumo ya watu wengine, kukosekana umeme, kuingiliwa kwa data kwa makosa au wizi, virusi vya kompyuta au mifumo ya wengine; uharibifu wa mipango; au uzembe wetu;
e. Uingiliaji, kutofanya kazi, ucheleweshaji au uharibifu mwingine wa bidhaa au huduma zinazotolewa na wengine pamoja na, bila ukomo, mifumo ya wengine kama vile watoaji mfumo wa simu ya umma, watoaji huduma ya umeme, mamlaka za mitaa na mamlaka za ithibati; na
f. Tukio lolote ambalo kwalo hatuna kinga nalo.
g. Kila upande sharti uufahamishe upande mwingine katika muda wa kutosha ikiwa kutakuwa na jambo

nje ya uwezo wao kuhusiana na huduma za chaneli za kielektroni.

27. Ukiukaji

Tunaweza kukatisha utumiaji wako wa huduma ya benki ya kielektroni endapo utakiuka masharti muhimu ya mkataba huu.

28. Namna ya kutatua migogoro

Migogoro yote inayotokana na matumizi yako ya huduma ya kieletroni ya benki, tafsiri ya mkataba huu au jambo lolote ambalo kwa mujibu wa mkataba huu linahitaji makubaliano ya wahusika (ukiachia mbali kurejeshwa fedha inayodaiwa na Benki au pale ambapo nafuu ya haraka inaweza kupatikana katika mahakama yenye mamlaka sahihi) itaamuliwa kwanza kupitia majadiliano ya kirafiki. Iwapo majadiliano yatashindikana basi shauri litatatuliwa na msuluhishi kama inavyoelekezwa na sheria za Tanzania kadiri zinavyorekebishwa mara kwa mara.

29. Uwezo wa kuingia kwenye mkataba

Unatuhakikishia kwamba una uwezo wa kisheria kuingia na kuwajibika na mkataba huu. Yeyote chini ya umri wa miaka kumi na nane (18) sharti asaidiwe na msimamizi wake kisheria wakati wa kusoma mkataba huu. Kama una umri chini ya miaka kumi na nane(18) sharti uzungumze na msimamizi wako kisheria
au wazazi wako. Endapo huna hakika kama una uwezo wa kisheria kuingia kwenye mkataba huu, sharti uwasiliane na mtu ambaye anaweza kukupatia taarifa hii kabla hujaendelea kutumia huduma ya kibenki ya kielektroni. Kituo cha Huduma kwa Wateja kitaweza kukusaidia katika jambo hili.

30. Sheria zinazosimamia uhusiano wetu

Mkataba huu utasimamiwa na kutafsiriwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania bila kurejea vipengele vyovyote vya migogoro ya kisheria.

31. Vipengele vya jumla


Vichwa vya ibara za mkataba huu vimewekwa tu kwa ajili ya ufanisi na urahisi wa rejea tu na visitumike kutafakari, kurekebisha au kupanua mkataba huu. Pale ambapo tarehe au nyakati vinahitaji kuhesabiwa kwa mujibu wa mkataba huu kipimo cha Muda wa Kimataifa (GMT) hutumika. Inapotokea migogoro kutokana na upekee wa mfumo wa mawasiliano, sote tunaruhusu mahakama au upatanishi, kadiri itakavyokuwa, kutafsiri mkataba huu kwa namna ambayo utawezesha shughuli za kawaida za kibenki bila kuweka mkazo usio wa lazima kwenye masuala ya kiufundi. Kushindwa au kuchelewa kwetu kwa aina yoyote kutekeleza haki zetu zozote kusichukuliwe kama kuachia haki hiyo, iwe imefanywa kwa dhahiri au fahamifu. Aidha haitaathiri uhalali wa sehemu yoyote ya masharti haya au kuathiri haki yetu ya kuchukua hatua yoyote dhidi yako. Iwapo maelezo, masharti au vipengele vyovyote vinaamuliwa kuwa havifai, batili au havitekelezeki kwa kiwango chochote kile; maelezo, masharti au kipengele hicho vitaondolewa kutoka kwenye maelezo, masharti au vipenge ambayo vitaendelea kuwa halali kwa ukamilifu kadiri ilivyoruhusiwa na sheria. Endapo una maswali yoyote katika mkataba huu, tafadhali wapigie Kituo chetu cha Huduma kwa Wateja.

Nimesoma, kuelewa na kuridhia maelezo na masharti haya.

Saini: _____

Tarehe: _____

Alama ya Dole Gumba



Bandika Picha

